**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Simu Na: +255 (026) 2963309/13/14
Nukushi: +255 (026) 2963316
Barua Pepe: ps@lands.go.tz
Tovuti: www.lands.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
2 Mtaa wa Ardhi,
S.L.P. 2908,
**40477 DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

## TANGAZO LA UUZAJI WA VIWANJA ENEO LA MALALUA - MLANGALINI HALMASHAURI YA WILAYA ARUSHA

**19 Julai, 2026 Dodoma**
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inautangazia umma kuwa, inauza viwanja katika barabara ya Afrika Mashariki (*East Africa bypass*) eneo la Malalua-Mlangalini Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

Bei ya viwanja katika mradi wa viwanja Malalua kwa mita ya mraba ni kama ifuatavyo:- Makazi (TZS 20,000), Makazi na Biashara (TZS 25,000), Biashara (TZS 30,000), Makazi ya Jumla (TZS 25,000), Shule (TZS 20,000), Kituo cha Elimu (TZS 20,000), Shamba la Mjini (TZS 15,000), Jengo la Umma (TZS 20,000), Matumizi ya Ibada (TZS 20,000), Hoteli (TZS 30,000), Viwanda vya Huduma (TZS 30,000), Camp Site (TZS 30,000), Kituo cha Mafuta (TZS 35,000), Kituo cha Biashara (TZS 30,000) na Kituo cha Afya (TZS 20,000).

Fomu za maombi zitatolewa katika Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Arusha tarehe **3 Agosti, 2026** kuanzia **saa tatu (3:00)** asubuhi hadi **saa tisa na nusu** (9:30) alasiri kwa gharama ya kiasi kiasi cha TZS 20,000/= (ambacho hakitarudishwa**). Fomu zitatakiwa kurejeshwa ndani ya siku kumi na nne (14) zikiwa zimejazwa kikamilifu pamoja na picha ya mwombaji ikiambatishwa pamoja na nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) pamoja na uthibitisho wa malipo ya asilimia ishilini na tano (25%) ya thamani ya kiwanja.**

**Waombaji waliokubaliwa watatakiwa kukamilisha gharama zote za ununuzi wa kiwanja ndani ya siku sitini (60) tangu tarehe ya kupewa namba ya malipo (*control number*). Endapo mwombaji atashindwa kukamilisha malipo ndani ya muda uliotolewa, atahesabika amevunja masharti na kiwanja husika kitatolewa kwa mtu mwigine bila ilani yoyote kwa mhusika.**

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Wizara ya *www.lands.go.tz* au kwa ufafanuzi zaidi piga kituo cha huduma kwa wateja kupitia namba ***0262161610***, ***0739646885, 0736665533*** au ***0659548000***.

**Imetolewa na:**

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
**WIZARA WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**